SWAHILI FORUM 11 (2004): 92-105

ATHARI ZA MABADILIKO YA MITAALA YA KISWAHILI KATIKA UANDISHI NA UCHAPISHAJI

NATHAN OYORI OGECHI

The present article attempts to analyse the effects of Kiswahili curricula changes in Kenya on Kiswahili authorship and publishing since 1963. The bottomline of the argument is that any changes on the educational curriculum affecting Kiswahili has a corresponding effect on the way Kiswahili authors and publishers behave. The analysis is divided into several periods marked with the various commissions appointed by the government to investigate and make recommendations on education. Based on the foregoing, the paper shows how the authors and publishers are compelled to adjust their attitude towards Kiswahili in order to keep abreast with the ever-changing millieu – at one time they cherish Kiswahili while discounting it at another. Finally, it is argued that at present there is a lot of good will towards Kiswahili. This can be enhanced if special incentives such as awarding higher entry salaries to applicants for jobs in the civil service who can fluently express themselves in Kiswahili.

1. Utangulizi

Imepita miaka 41 tangu Kenya ijishindie uhuru kutoka kwa ukoloni wa Mwingereza. Uhuru huo ulikuwa si wa kisiasa tu bali pia wa kiuchumi na kiutamaduni. Utamaduni umejumuisha mambo mengi elimu ikiwa ni mojawapo wa mambo hayo. Katika kipindi hicho cha miongo minne, mabadiliko mengi yametokea katika elimu. Mabadiliko hayo hasa yamejikita katika mitaala kwa jumla na katika mitaala ya Kiswahili kibayana.

Katika makala hii, tunajaribu kutathmini athari za mabadiliko haya ya mitaala ya Kiswahili katika uandishi na uchapishaji. Anavyodai Altbach[1] (1999: 2 – 3):

> …..skuli, pamoja na taasisi za elimu ya juu, hutegemea vitabu na machapisho mengine ili kuyatimiza malengo ya kielimu. Uhusiano wa kutegemeana unadumu kati ya uchapishaji na mfumo wa elimu katika viwango vyote.

Kwa hivyo, patokeapo mabadiliko yoyote ya kimitaala katika elimu vivyo hivyo panatokea mabadiliko ama chanya au hasi katika uandishi na uchapishaji. Uandishi ni mfanyiko ambao unahusiana na utungaji wa vitabu (vya kiada na ziada), magazeti, utungaji mashairi magazetini n.k. Kwa hivyo, uandishi katika lugha yoyote ile unategemea kuwepo kwa watunzi wa miswada katika maeneo haya yote ili miswada hiyo ifanyiwe uchapishaji. Kwa upande mwingine, katika mtazamo finyu, uchapishaji ni mfanyiko changamano kwani unahusu kuifanya miswada ya watunzi iwe vitabu, majarida, magazeti n.k. Lakini kiupana, uchapishaji pia unawajumuisha waandishi, wachapaji, wauzaji vitabu, wakutubu n.k.

Uchangamano wa mifanyiko hii miwili unaonyesha kuwa kufaulu au kufeli kwa shughuli hizi hutegemea kuwepo au kutokuwepo kwa wasomaji na uwezo wa wasomaji hao kuyanunua

[1]Nimetoa tafsiri za kazi zote zisizo za Kiswahili ambazo zimenukuliwa katika makala hii.

machapisho (Mulokozi 1999; Chakava 1996; Rotich 2000). Uwezo huo wa kununua unaweza kuwa ama wa msomaji binafsi au maktaba za vyuo au umma. Isitoshe, usomaji pia unategemeana na kuathiriana na uchapishaji. Mathalani, wasomaji wanaweza kuwepo na maktaba zikawepo lakini maktaba zile zikawa na machapisho katika lugha ama ya wasemaji wachache katika nchi ile au lugha ambayo watu hawakuitumia katika elimu na hivyo hawapendi kuisoma.

Kwa ujumla, tunadai kuwa uandishi, uchapishaji na mitaala vinategemeana na kuathiriana. Katika uchangamano huo maswali kadha wa kadha huibuka: Je, kumetokea mabadiliko yoyote katika sera ya lugha na mitaala nchini Kenya? Mabadiliko hayo yamepelekea kuwepo kwa wasomaji nchini Kenya? Iwapo wapo, wanasoma katika lugha zipi? Wapo watungaji wa Kiswahili? Vipo viwanda vya wachapishaji na wachapaji nchini? Vipo viwanda na wapo waandishi? Wametoa machapisho kiasi gani katika Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu?

Makala hii basi inajaribu kutathmini ni vipi mabadiliko katika mitaala inayohusiana na Kiswahili yanaathiri washika dau katika mfanyiko wa uchapishaji kwa Kiswahili. Hususan makala hii inajikita katika uandishi na uchapishaji katika shule za chekechea, vitabu vya kiada na ziada katika shule za msingi na za upili na vile vya elimu ya watu wazima. Viwango hivi vya elimu vimechaguliwa kwa sababu tunahisi kuwa wanafunzi wa viwango hivi ama wanapewa msingi wa kujifunza na kupendelea kukisoma Kiswahili (chekechea, shule za msingi na sekondari) au wanajifunza na kuendelea kukuza ujuzi wao wa kukisoma Kiswahili kikiwa ni lugha inayotumika sana katika maisha yao ya kila siku (elimu ya watu wazima). Data iliyotumika hapa imetokana na uchunguzi wa maandishi mbali mbali pamoja na katalogi za viwanda vya uchapishaji.

Makala hii ina sehemu sita. Sehemu ya pili inaangazia hali ya kiisimu-jamii nchini Kenya. Mabadiliko ya sera ya lugha yaliyoathiri mitaala ya Kiswahili pamoja na kuwepo au kutokuwepo kwa wasomaji wa Kiswahili vimeshughulikiwa katika sehemu ya tatu. Kisha, sehemu ya nne inamulika hali ya waandishi na viwanda vya uchapishaji nchini. Usasambuzi wa kuwepo kwa machapisho ya Kiswahili katika viwango mbalimbali unajitokeza katika sehemu ya tano. Hatimaye, hitimisho linatolewa katika sehemu ya sita.

2. Hali ya kiisimu-jamii nchini Kenya

Kenya ni taifa changamano kiisimu-jamii. Nchini humo mnaishi watu milioni 30 wa asili za Kiafrika, Kiasia, Kiarabu na hata Kizungu. Idadi ya lugha zinazosemwa na watu hao ni kubwa na ni vigumu kuitaja wazi wazi. Ugumu huo unatokea kwa sababu ni muhali kuweka mpaka kati ya dhana za lugha na lahaja (Hudson 1980). Ugumu mwingine umejikita katika siasa ambapo jamii kama vile Wasuba waliochukuliwa kuwa lahaja ya Waluo hapo awali sasa wamefufuliwa kilugha na kupewa hadhi ya lugha (Kembo-Sure 2000: 646). Pia imedaiwa kuwa lugha nyingine 16 ama zimetoweka au zimo katika ukingo wa kutoweka. Mwisho, machapisho mbalimbali yanataja idadi tofauti ya lugha (Ogechi 2003). Kwa mfano, machapisho

mengi hudai kuwa idadi ya lugha nchini Kenya ni 43 (Whiteley 1974; Heine 1977; Chakava 1995, Republic of Kenya 1999, Webb & Kembo-Sure 2000). Lakini Githiora (2002: 162) anataja lugha 60 ilhali kielelezo cha katiba ya Kenya (CKRC 2002) kinadai idadi hiyo ni 70. Iwapo madai kwamba Sheng[2] sasa inaelekea kuwa ni lugha yenye wazawa asili (Ngesa 2002; Kiessling & Mous 2001, Githiora 2002) basi idadi ya lugha itakuwa ni kubwa. Vyovyote iwavyo, makala hii itachukulia kuwa 43 ndio idadi ya lugha nchini Kenya.

Lugha za Kiafrika zimegawika katika makundi matatu makuu. 65% yao ni Wabantu, k.v. Waswahili, Wakikuyu, Abagusii n.k. (Myers-Scotton 1993, Githiora 2002), 30% ni Wanailotiki k.m. Waluo, Wakalenjin, Wamaasai ilhali 3% ni Wakushitiki k.m. Waborana, Wasomali, Warendille n.k. Lugha tano kuu zimetawanyika ifuatavyo: Kikikuyu (20%), Kiluo (14%), Kiluyia (13%), Kikalenjin (11%) na Kikamba (11%) (Webb & Kembo-Sure 2000).

Katika hali ya wingi-lugha kama hii, ni lazima patafutwe suluhu jinsi ya kuzitumia lugha hasa katika mazingira ya umma. Kwa hivyo, sera ya lugha iliyopo ni kuwa Kiingereza ndio lugha rasmi inayotumiwa bungeni, utumishi wa umma, ubalozi, elimu ya juu, biashara za kimataifa, sheria n.k. Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi (Myers-Scotton 1993; CKRC 2002; Ogechi 2003; Githiora 2002). Lugha za kikabila hutumika tu katika kuanzisha elimu ya watoto shuleni na elimu ya watu wazima (Republic of Kenya 1999). Hata hivyo, katika sehemu za mashambani hali halisi inaonyesha kuwa lugha hizo za kikabila pamoja na Kiswahili zinatumiwa kufundishia hadi darasa la mwisho la shule za msingi (Wolff 2002).

3. Mabadiliko ya mitaala na wasomaji nchini Kenya

3.1 Mitaala

Dhana ya mtaala ni changamano na imeelezwa kwa namna mbalimbali na wataalamu tofauti wa elimu. Kwa mfano, Bobbit (1968 katika Okech & Asiachi 1992) amedai kuwa mtaala ni ule mfululizo wa vitu ambavyo watoto na vijana ni lazima wavifanye na wavipitie maishani mwao kama njia mojawapo ya kukuza uwezo wao wa kufanya kimwafaka mambo ambayo ni ya kiutu-uzima. Naye Beauchamp (1968 katika Okech & Asiachi 1992) ameeleza kuwa mtaala ni kozi/masomo na yaliyomo katika kozi hizo. Hususan amedai kuwa mtaala ni hati iliyoandikwa ambayo inajumuisha viambato, lakini hasa mpango wa elimu ya watoto wanapokuwa wamesajiliwa katika shule fulani. Kufuatia madai ya wataalamu hawa wa awali, Okech & Asiachi (1992:4) wameeleza mtaala kuwa:

> ...mpangilio wa matendo yaliyonuiwa kumfanya mwanafunzi atimize kadiri inavyowezekana malengo fulani ya kielimu. Katika hali finyu mtaala ni masomo ya-

[2] Sheng ni msimbo usiokuwa thabiti unaosikika kama Kiswahili ambao hutumiwa miongoni mwa vijana (Ngesa 2002). Sheng ina msamiati wa kipekee ambao pia si thabiti. Inazungumzwa sana na vijana mijini na miongoni mwa vijana mashambani (Ogechi 2002: 4):

Kithora ma-doo z-a mathee
ku.iba NGL6-dough NGL10-KIUNG mother
'to steal my mother's money' (Abdulaziz & Osinde 1997:56)
'kuiba pesa za mama'

> nayofundishwa, au kiupana mtaala ni matukio anayoyapitia mwanafunzi nje na ndani ya skuli.

Ili kuuendesha mjadala wa makala hii, tunachukulia mtaala katika ufinyu na upana wake. Maanake tutachukulia mtaala kama matukio shuleni ambapo panafundishwa kozi mbalimbali huku Kiswahili kikiwa mojawapo. Pia tutachukulia matukio nje ya shule kama vile uandishi na uchapishaji wa vitabu, magazeti, majarida n.k. mbalimbali kwa Kiswahili vinavyouzwa na wauzaji tofauti au kununuliwa na watu binafsi na maktaba tofauti tofauti pamoja na matumizi ya Kiswahili maishani mwa mwanafunzi kama ni mtaala. Vyote hivyo humsaidia mwanafunzi kujiimarisha kielimu. Wanafunzi wetu hapa ni wa shule za chekechea, msingi, upili, na elimu ya watu wazima.

Mabadiliko ya kimitaala yanayohusiana na uandishi na uchapishaji wa Kiswahili yanahusiana na mabadiliko ya mifumo ya elimu nchini Kenya. Mfumo wa elimu unapobadilika unaathiri masomo mengi. Hata hivyo, katika makala hii tutalenga mabadiliko yaliyohusiana na Kiswahili pekee. Tutajikita katika mabadiliko hayo tangu uhuru hadi leo (2004).

Mnamo 1964 serikali iliteua Tume ya Elimu ya Kenya iliyoongozwa na Prof. Ominde. Tume hiyo ilipendekeza mfumo wa elimu wa 7-4-2-3[3]. Pia ikapendekeza matumizi ya Kiingereza katika kufundishia tangu shule za msingi. Kutekelezwa kwa pendekezo hilo kulipelekea kuanzishwa kwa Mwelekeo Mpya wa Msingi. Hata hivyo, tume ikatahadharisha kwamba lugha za kikabila zisipuuzwe. Kwanza, ikapendekeza pawepo na angalau kipindi kimoja cha *fasihi simulizi* (kutoa hadithi) kila siku katika ratiba ya shule kati ya madarasa ya 1 na 3. Pia Kiswahili kilitambuliwa kama lugha ya taifa na utaifa wa Afrika. Kwa sababu hiyo, tume ikapendekeza mpango maalum wa kuwaandaa walimu wa Kiswahili na Kiarabu nyakati za likizo. Hata kama Kiswahili kilitambuliwa, ufundishaji wake katika skuli za msingi haukutiliwa maanani. Kilitengewa vipindi vichache sana na hakikutahiniwa katika mtihani wa mwisho wa darasa la saba – Certificate of Primary Education (CPE). Kwa hivyo, shule nyingi hazikukifundisha kamwe na vipindi vyake vikatumiwa kwa ajili ya masomo muhimu k.v. Hisabati na Kiingereza (Ogechi 2002b).

Kufikia 1967, shule nyingi hasa za mashambani zilikumbwa na matatio kufuata Mwelekeo Mpya wa Msingi na zikaanza kufundisha kwa lugha za kikabila. Mwelekeo Mpya wa Msingi ukapuuzwa na kukaanza kufundishwa lugha za kikabila kwa miaka ya kwanza mitatu ya shule za msingi. Mtaala huu uliathiri ufundishaji wa lugha za kikabila na hivyo kitengo cha Mbinu za Kijumla katika Taasisi ya Elimu ya Kenya (Kenya Institute – KIE) kilianzisha uchapishaji wa mfululizo wa vitabu katika lugha za kienyeji ulioitwa *Tujifunze Kusoma Kikwetu*. Kufikia 1970, mkazo uliotiliwa Mwelekeo Mpya wa Msingi ulilegezwa kwa sababu ya ukosefu wa usare katika ufundishaji, marejeleo na ukaguzi mbaya wa ufundishaji shuleni.

[3] 7-4-2-3 ina maana: miaka saba ya masomo ya shule ya msingi, minne katika shule ya upili, miwili katika kiwango cha juu cha shule ya upili na angalau mitatu katika chuo kikuu.

Athari kubwa ya mabadiliko ya mitaala kufuatia Tume ya Ominde (1964) mintarafu ya uandishi na uchapishaji imeelezwa na Chakava (1992a: 121):

> …ingawa vitabu ni nguzo muhimu katika ufanisi wa mfumo wowote wa elimu, ripoti ya tume haikusema lolote kuvihusu na jinsi ambavyo vingetungwa, vikazalishwa na kusambazwa ili kuutumikia mfumo wa elimu uliopendekezwa. Na kwa kuwa ripoti hii muhimu haikusema lolote, nafasi muhimu ya kupendekeza sera ya taifa kuhusu uchapishaji wa vitabu na usambazaji wao ilipotezwa.

Mtaala tena ukabadilika mnamo 1976 kupitia kwa tume ya serikali iliyoongozwa na Gachathi (Republic of Kenya 1976). Tume hiyo ikapendekeza ufundishaji kwa lugha za kikabila hadi darasa la tatu. Pia ikapendekeza ufundishaji na utahini wa Kiswahili katika mtihani wa CPE. Hata hivyo, mintarafu ya Okech & Asiachi (1992:135) "bado tutaendelea kukitumia Kiingereza kama lugha ya taifa na lugha ambayo kwayo vifaa vyote vya kufundishia vitatungwa". Labda kwa sababu hii na nyinginezo za kisiasa[4] Kiswahili hakikutahiniwa katika mtihani wa CPE. Vipindi vyake bado vikaendelea kutumiwa kufundishia masomo muhimu. Katika shule za upili, Kiswahili kilikuwa somo la hiari na skuli nyingi hazikukifundisha.

Mnamo 1981 aliyekuwa rais wa Kenya, Mhe. Daniel arap Moi, aliunda tume iliyoongozwa na Mackay (Republic of Kenya 1981). Tume hii ilipendekeza mtaala ambao unabobea mwelekeo wa kiufundi badala ya ule wa awali uliokuwa wa kinadharia. Mfumo wa awali ulimtayarisha mwanafunzi kuishinda mitihani tu na kutafuta kazi za utepe mweupe. Ikapendekezwa kuwa mfumo wa elimu ubadilike kutoka 7-4-2-3 hadi 8-4-4[5]. Isitoshe, ili kuhakikisha kuwa ufundi umeufikia umma, ikatakiwa lugha ya Kiswahili isisitizwe. Hii hasa ilitokana na ugunduzi kuwa wengi wa wanafunzi waliofuzu kutoka vyuo vikuu hawangeweza kujieleza kwa Kiswahili (Republic of Kenya 1981: 40). Basi ikawa Kiswahili ni somo la lazima la kufundishwa na kutahiniwa katika mitihani ya shule za msingi na sekondari.

Alivyodai Mukuria (1995) Kenya ilijikuta haina vifaa (vitabu na walimu wa Kiswahili) vya kutekeleza pendekezo hili. Mitaala ya awali ilifanya wachapishaji kutopendelea kupokea miswada ya Kiswahili kwa kuwa soko la lugha hii lilikuwa finyu. Mitaala ilihimiza uandishi na uchapishaji kwa Kiingereza kama kielelezo 1 kinavyoonyesha:

[4] Wanasiasa waliokuwa na ushawishi mkubwa wakati huo kama vile Mkuu wa Sheria, Charles Njonjo, walikuwa wanakipiga vita Kiswahili na kudai kuwa hakikuwa lugha ya Kiafrika na kwamba hakingeweza kutumika katika taaluma.

[5] 8-4-4 ina maana ya miaka minane ya shule ya msingi, minne ya shule ya upili na angalau minne ya chuo kikuu.

Kielelezo 1: Vitabu vilivyochapwa kulingana na lugha (Publishers Register; Department of the Registrar General, Office of the Attorney General, Nairobi)

Mwaka	Jumla	Lugh Kisw
1977	71	17
1978	92	22
1979	84	13
1980	93	31

Mnamo 1999, kufuatia matamko na malalamiko mengi ya wanasiasa kwamba mfumo wa 8-4-4 ulikuwa haupigi ndipo, serikali ikaunda tume ya uchunguzi ya elimu ya Kenya chini ya uongozi wa Davy Koech (Republic of Kenya 1999). Tume hii ilitoa mapendekezo ambayo yalitaka 8-4-4 ipuuziliwe mbali na kurudishwa mfumo wa 7-4-2-3. Lakini ikasisitiza kwamba Kiswahili bado kiendelee kufundishwa na kutahiniwa. Kwa mara ya kwanza tume hii ikataka elimu ya chekechea ipewe umuhimu kwani awali ilikuwa haipewi umuhimu na serikali.

Serikali haikuyatekeleza mapendekezo ya tume hiyo moja kwa moja[6]. Nayo serikali mpya ya NARC[7] mnamo Oktoba 2003 iliandaa kongamano la elimu jijini Nairobi ambalo lilitathmini mfumo wa elimu. Ijapokuwa wananchi walitarajia kuwa marekebisho makubwa yakijumuisha kubadili mfumo wa 8-4-4 yangetangazwa, hakuna jipya lililojiri. Badala yake wajumbe waliafikiana kufanya uchunguzi zaidi na pia kufanya marekebisho pale ambapo walihisi kwamba 8-4-4 ilikuwa na ulegevu.

Tume hizi zote zilitoa mapendekezo ambayo yalikuwa na athari kwa uandishi na uchapishaji wa Kiswahili ambayo yanajadiliwa katika makala hii.

3.2 Wasomaji wa Kiswahili

Je, mabadiliko ya mitaala yaliyotokea tangu uhuru yamezaa wasomaji wa Kiswahili kibayana na wasomaji kwa ujumla? Kung'amua idadi kamili ya wasomaji nchini Kenya huweza kukisiwa kwa kurejelea kiwango cha uwezo wa kusoma na kuandika. Hapa vile vile tunapata ugumu kwa sababu ya tofauti zilizopo kuhusu ujuzi huu katika maandishi k.v. 54% (Makotsi & Nyariki 1997), 75% (Callaghan 1997), 69% (Article 19 1999), 70% (Republic of Kenya 1999) au 50% (Ministry of Finance and Planning 2002). Isitoshe, waliotafitia suala hili wanadai kuwa tabia za usomaji nchini Kenya ni hafifu (Odaga 1997; Rotich 1997) ingawa tunaweza kudai kuwa kwa yakini wasomaji (bila kujali lugha wanayoisoma) wapo. Jambo ambalo ni gumu kulitaja ni idadi ya watu wanaokisoma Kiswahili.

[6] Baadhi ya mapaendekezo ya tume hiyo kama vile kupunguza idadi ya masomo ya kutahiniwa katika shule za msingi na upili yalitekelezwa.

[7] NARC inawakilisha National Rainbow Alliance.

Ijapokuwa Mulokozi (2002 katika mtandao wa Chuo Kikuu cha Helsinki) anadai kuwa wapo watu 20,000,000 wanaokizungumza Kiswahili nchini Kenya, hatuwezi kusema kwa yakini ni idadi ya watu wangapi kati yao wanaoweza kukisoma Kiswahili. Hii ni kwa kuwa lugha ya kufundishia ni Kiingereza na wala si Kiswahili. Isitoshe, mielekeo ya Wakenya kwa ufundishaji wa Kiswahili ni hasi. Kwa mfano, Bota (2002), aliyeshughulikia utekelezaji wa mtaala wa elimu ya kipekee nchini Kenya, aligundua kwamba wanafunzi na walimu katika shule za kipekee nchini wanachukuliwa ufundishaji wa Kiswahili kama ni kupoteza muda na wakapendekeza kuwa somo hili liondolewe katika mtaala wa masomo yao. Labda sababu hii ndio ilimfanya Mulokozi (1999: 15) kuhitimisha:

Wakenya wengi wanaojua kusoma na kuandika, na wenzao wote kutoka Tanzania, wanaweza kukisoma Kiswahili. Kwa hivyo, idadi kubwa sana ya wasomaji wa vitabu vya Kiswahili ipo nchini Kenya na Tanzania. Tatizo la usomaji basi halihusiani na ukosefu wa wasomaji, bali linahusiana na suala la ufaafu, ukubalifu, utoaji wa bei (ya vitabu kulingana na uwezo wa wasomaji wa kuvinunua) pamoja na ukuzaji na usambazaji wao kwa jumla.

4. Waandishi na viwanda vya uchapishaji

Tumezungumzia Kenya na Tanzania pamoja kwa sababu kuna mtegemeano mkubwa katika uandishi na uchapishaji kati ya nchi hizi mbili (Ogechi 2003a). Tatizo la waandishi kilugha limeelezwa na Chakava (1992b: 34):

> ….kiungo kati ya mwandishi wa kiafrika na hadhira yake kimelegezwa sana na suala iwapo ataandika katika lugha yake ya mzazi (kila nchi ina lugha nyingi) au katika lugha ya kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa au Kireno, ambapo atawasiliana na idadi ndogo sana ya watu. Inaelekea kuwa lugha za kigeni kwa sasa zinatoa nafasi kubwa ya ufanisi kuliko lugha za kienyeji. Hata hivyo, ni heri itajwe kuwa lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili zinaweza kufanya mawasiliano ya kiufundi na kisayansi. Kwa hivyo, inaweza kuwa lugha mwafaka ya kuleta utamaduni wa kisayansi barani Afrika.

Hata hivyo, tunaona kuwa waandishi wa vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa nchini Kenya huwa ama ni Wakenya au Watanzania (Ogechi 2002a; Mbaabu 1996). Idadi yao kamili haijulikani. Hata hivyo, Mulokozi (1999: 17-18) anakisia kuwa idadi ya wale wanaotunga vitabu vya kiada na ziada ni zaidi ya 3,000. Anaendelea kueleza kuwa iwapo tutazungumzia watunzi wa mashairi, hadithi fupi zinazochapishwa magazetini, pamoja na watunzi wa tamthilia zinazoigizwa jukwaani, basi tutakuwa tunazungumzia takriban waandishi 10,000 wa Kiswahili. Basi hakuna ukosefu wa waandishi wa Kiswahili.

Historia ya viwanda vya uchapishaji nchini Kenya na Tanzania imezungumziwa kwa mapana na marefu (Chakava 1995; Makotsi & Nyariki 1997; Callaghan 1997; Mulokozi 1999). La muhimu ni kuwa uchapishaji katika nchi hizi umeanza mnamo karne ya 19 (kwa maelezo marefu tazama Callaghan 1997; Ogechi 2002b, Mulokozi 1999). Katika siku za awali haingewezekana kutenganisha kati ya uchapishaji na uchapaji (Mulokozi 1999: 12). Jambo jingine ni kuwa viwanda vya uchapishaji nchini Kenya ama ni vya kimataifa, mashirika ya serikali na vile vya kibinafsi. Mulokozi (1999: 14) amehitimisha:

Leo hii, zaidi ya viwanda vya uchapishaji 130 vimesajiliwa nchini Kenya na 150 nchini Tanzania. Vile vinavyoongoza nchini Kenya ni JKF, Kenya Literature Bureau (KLB), Longman, Oxford University Press (OUP), East African Educational Publishers (EAEP), Phoenix na Lake Publishers. Vinavyoongoza nchini Tanzania ni: Tanzania Publishing House (TPH), Eastern Africa Publications Ltd. (EAPL), Dar es Salaam University Press, Ben and Company, Press and Publicity Centre, OUP, Ndanda-Peramiho Mission Press, Mkuki na Nyota na Heko Publications.

Inashangaza kuwa University of Nairobi Press, Moi University Press na Maseno University Press si mojawapo wa wachapishaji maarufu huku tukizingatia kuwa kama sehemu ya vyuo vikuu (ambavyo ni chemi chemi ya miswada), viwanda hivi vingetarajiwa kuwa vinatoa machapisho mengi. Labda hali hii inatokana na athari za mitaala ya Kiswahili. Sera ya uchapishaji katika viwanda hivi ni kupokea, kuhariri na kuchapisha vitabu vinavyotumiwa kufundishia katika vyuo vikuu. Kumbuka lugha ya elimu ya juu nchini Kenya ni Kiingereza na wala si Kiswahili. Kiswahili kinafundishwa tu kama mojawapo ya taaluma katika chuo kikuu. Kwa hivyo, vitabu vichache vilivyochapishwa na wachapishaji wa chuo kikuu kama vile Moi University Press na University of Nairobi Press ni vile tu ambavyo vinafaa mahitaji ya ufundishaji katika chuo kikuu.

Kabla ya kuchunguza viwango vya uchapishaji kwa Kiswahili katika viwango mbalimbali ni muhimu kuelezea uhusiano mbaya uliodumu kati ya viwanda vya kibinafsi na serikali. Uhusiano huo mbaya uligusiwa na Chakava (1992b: 33):

> …viwanda vya uchapishaji vya kiafrika havijajumuishwa katika mikakati ya maendeleo ya kitaifa. Mikopo ya Benki ya Dunia kwa serikali za kiafrika kwa ajili ya kuendeleza vitabu hutumiwa katika miji mikuu badala ya kuimarisha uwezo wa kule mashambani. Ningependa kuwaomba marafiki zetu wenye huruma kutoka Kaskazini watusaidie katika kuzibembeleza serikali zetu zibadili mwelekeo huu, kwani wao ndio washauri na watekeleza miradi ya Benki ya Dunia na hata kwa serikali zetu. Wachapishaji wa kiafrika hawana mikondo mingi ya kuwasiliana na serikali zao ambazo hazijali matatizo yao.

Uti wa mgongo wa uchapishaji barani Afrika ni vitabu vya kiada. Kila kampuni ingependa kuchapisha na kuuza vitabu hivi. Lakini tangu uhuru TEK ilikuwa inaandaa miswada ya vitabu vya kiada ambavyo vilichapishwa na KLB na JKF (iliyoundwa mnamo 1965). Serikali pia iliunda KSES ili ivinunue vitabu na kuvisambaza kwa skuli zote nchini. Kwa hivyo, si wachapishaji wa kibinafsi wala wauzaji wa kibinafsi walifaidi kutoka kwa sekta hii. Sera hii iliendelea hadi 1999 ambapo wizara ya elimu ilitoa mwongozo mpya (Rotich 2000). TEK ilikoma kuandaa miswada. Kila kampuni ya uchapishaji ingeandaa vitabu ambavyo vingechunguzwa na TEK na orodha ikapendekezwa. Somo moja lingeweza kuwa na orodha ya vitabu kadhaa vilivyopendekezwa. Kisha kamati za skuli zingeweza kuteua vitabu vya kununua kutokana na orodha hiyo. Kamati ziliwajumuisha walimu wa skuli na wanachama wawili wa halmashauri ya wazazi. Hatua hii imeng'oa ukiritimba wa serikali.

5. Uandishi na uchapishaji katika viwango mbalimbali

Kufikia sasa tumeona kuwa wapo waandishi, wasomaji na viwanda vya uchapishaji katika ukanda mnamotumiwa Kiswahili. Isitoshe, tumeonyesha sera ya lugha pamoja na mabadiliko ya sera/lugha ya mitaala kuhusiana na Kiswahili kwa miongo minne iliyopita. Katika sehemu hii, tungependa kuchanganua na kuona ni vipi mabadiliko hayo yalivyoathiri uandishi na uchapishaji katika Kiswahili. Tutafanya uchambuzi wetu kwa kuzingatia ngazi mbalimbali za elimu.

5.1 Shule za chekechea na vitabu vya watoto

Kama tulivyoonyesha, shule za chekechea hazikujumuishwa katika mabadiliko ya kimitaala ya serikali isipokuwa tu katika tume iliyoongozwa na Koech (Republic of Kenya 1999). Anavyodai Jwan (2004), leo hii shule nyingi za chekechea zinazingatia mfumo wa Kimontessori. Katika mfumo huu, mwanafunzi anafundishwa kujumuika na kuingiliana na wenzake. Mtaala wao unawafundisha kuimba, kuhesabu, kuandika numerali na stadi za lugha. Msisitizo huwa ni matumizi ya lugha kwa jumla. Lugha pekee iliyotajwa ni lugha ya mzazi (KIE 2000: 33) – kuwa ni "kuhimiza watoto kupenda na kutumia lugha mama". Kiswahili hakikutajwa. Katika skuli za mijini wale watoto wanaoongea Kiswahili huadhibiwa kwa kuchekwa na wenzao kama wanavyoagiza walimu wa watoto hao (Ogechi 2003). Kwa sababu hiyo uandishi na uchapishaji kwa Kiswahili kwa ajili ya shule za chekechea haukushughulikiwa sana. Unahitaji kushughulikiwa kwa makini. Upekuzi tuliofanya katika katalogi za miaka 2000 hadi 2003 za wachapishaji maarufu nchini (k.v. Macmillan, East African Educational Publishers, Jomo Kenyatta Foundation na Kenya Literature Bureau) umeonyesha uhaba mkubwa wa vitabu vya shule za chekechea. Ni EAEP tu waliokuwa na vitabu vya kiwango hiki. Lakini vitabu hivyo pia havijatungwa na kuchapishwa maksudi kwa watoto hao. Vinaitwa "pre-primary and primary school books". Kwa hivyo, haviwalengi moja kwa moja.

Utungaji wa vitabu vya watoto kwa ujumla nchini Kenya haukufana hadi mwongo wa 1980 (Callaghan 1997). Sababu kuu labda ni kuwa wachapishaji wengi hawakuwa wamepata namna ya kuendesha biashara ya vitabu hivyo. Kwa mfano, Chakava (1998) alijaribu kuchapisha kazi za watoto katika mfululizo wa *Visa na Mikasa* mnamo 1987. Mradi huo uliambulia patupu licha ya kuwa vitabu hivyo vilikuwa vimependekezwa na wizara ya elimu kutumiwa shuleni. Labda kufeli kwa mradi huu kulitokana na ukweli kuwa mitaala ya Kiswahili haisisitizi Kiswahili katika kiwango cha watoto. Hata wazazi waliobobea kasumba kuwa Kiingereza kina hadhi hawawanunulii watoto wao vitabu vya Kiswahili. Pia vitabu vilikuwa vya bei ghali kwani vielelezo vilichapwa kwa rangi na karatasi ghali. Njia pekee ya kuimarisha sekta hii ni kutotumia vielelezo vya rangi na kuunda mifululizo mingine katika Kiingereza. Mifululizo ya Kiingereza itauzwa kwa bei ya juu ili faida inayopatikana itumike kuandaa vile vya Kiswahili. Kwa mfano, inadaiwa kwamba EAEP inauza nakala 3,000 kwa kila anwani ya vitabu vya watoto kwa kila mwaka:

Kielelezo 2: Vitabu vya watoto EAEP (Chakava 1998:4)

Vitabu kwa lugha za kikabila	Vita
Gikuyu	3
Dholuo	2
Luhyia	4
Kiswahili readers	-
Visa na Mikasa	9
Paukwa Pakawa	4
Vitabu vya Nyota	9
Vitabu vya Sayari	13

Mfumo huo pia unafuatwa na kampuni ya Sasa Sema ambayo ina mifululizo kadhaa k.v. Lion Books (*Jomo Kenyatta, Mekatilili wa Menza, Poetess from Lamu* na *Elijah Masinde*). Pia vipo vile vyenye vielelezo k.v. *Abunuwasi, Manywele, Macho ya Mji, Mbegu ya Ajabu* na *Ndoto ya Amerika.*

5.2 Vitabu vya kiada

Vitabu hivi ndivyo uti wa mgongo katika uandishi na uchapishaji (Chakava 1996; Makotsi & Nyariki 1997, Mulokozi 1999). Kama tulivyodai awali (Ogechi 2002c), iwapo tungependa kuimarisha utungaji na uchapishaji wa vitabu kwa Kiswahili, basi ni lazima Kiswahili kipewe hadhi katika mitaala. Ni lazima utahini wa Kiswahili uonekane kuwa unachangia katika kumsaidia mwanafunzi ajijenge kitaaluma. Kwa mfano, kule kufanya alama ama ya Kiswahili au Kiingereza katika KCSE kuchangia katika uteuzi wa wanafunzi wa vitivo k.v. tiba, uhandisi n.k. kumewahimiza waandishi na wachapishaji kukizingatia Kiswahili (Muruguru 2000). Isitoshe, anavyodai Mukuria (1995), mtaala wa Kiswahili ulioanzishwa na Tume ya Mackay (1981) ulikumbwa na matatizo ya ukosefu wa vitabu pale ulipoanzishwa rasmi kwa sababu wachapishaji walikuwa hawaikubali miswada ya Kiswahili. Lakini hali hii iliimarika baada ya muda wa mwongo mmoja kwani Kiswahili kilikuwa kimepanda hadhi. Kielelezo cha 3 kinaonyesha idadi ya vitabu vya Kiswahili ilivyoimarika baada ya Tume ya Mackay (1981).

Kielelezo 3: Vitabu vya kiada vilivyochapishwa (Chakava 1996: 32)

Lugha/Mwaka	1985	1986	1987	1988	1989	Jumla
Kiswahili	28	38	30	54	69	219
Nyingine - za kienyeji	2	5	3	9	25	44
Kiingereza	82	110	161	161	263	777
Nyingine - za kigeni	3	-	-	-	2	5
Jumla	115	153	194	224	359	1,045

Hali hii lazima imeimarika kufikia sasa kwani kufikia 1998 KIE ikitumia JKF na KLB ilikuwa na ukiritimba wa kuchapisha na kuuzia skuli vitabu (Rotich 2000a) kama tulivyokwisha onyesha. Tangu mwaka huo, mpango wa Benki ya Dunia uliilazimisha serikali kuyaruhusu mashirika mengine ya kibinafsi kushiriki katika uchapishaji wa vitabu vya kiada. Kwa kuwa vitabu hivyo pia vingeteuliwa na skuli zikaruhusiwa kuvinunua upo uwezekano kuwa makampuni mengi ya kibinafsi yanachapisha vitabu vya Kiswahili.

5.3 Vitabu vya elimu ya watu wazima

Kuna viwango viwili katika elimu ya watu wazima: utangulizi kwa elimu hii ambapo wanafunzi hutumia lugha za kikabila na kiwango cha pili ambapo wale waliohitimu kiwango cha kwanza wanajiendeleza zaidi. Katika kiwango cha chini palikuwa na jaribio la kutumia Kiswahili kwanzia 1972 lakini mradi huo ulifeli (Ogechi 2002a) na lugha 17 za kikabila zinatumika. Hamna sera thabiti ya serikali kuhusu lugha katika kiwango cha juu cha elimu ya watu wazima katika ufundishaji, utungaji na uchapishaji (Owino 1999). Kwa mfano tangu 1996, serikali ikishirikiana na shirika lisilokuwa la serikali la Ujerumani, GTZ, imekuwa ikiendesha mradi wa kutunga, kuandaa na kusambaza machapisho ya kiwango cha juu cha kisomo hiki katika wilaya 12. Wanafunzi wanajumuishwa katika uandishi wa vitabu hivi (Thompson 2001: 10) kwa kuchuma nafuu ya uchuzi wao wa kienyeji k.v. ufugaji, unyunyuziaji mashamba maji, ukuzaji wa nyuki n.k.

Kinachoshangaza ni kuwa utungaji na uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili si mkubwa. Kwa mfano, ripoti ya mwaka 2000 kutoka Korr, Wilaya ya Marsabit ilionyesha kuwa miswada sita iliandaliwa mwaka huo ambapo miswada mitano ilikuwa ya Kiingereza na ni mmoja tu uliokuwa wa Kiswahili ilhali hakukuwa na mswada hata mmoja kwa Kirendille. Baadaye, inadaiwa kuwa wenyeji walilalamika na kutaka miswada zaidi kwa Kirendille.

6. Hitimisho

Azma ya makala haya ilikuwa ni kuchunguza jinsi gani mabadiliko ya kimitaala kuhusu Kiswahili yanavyoathiri uandishi na uchapishaji kwa Kiswahili. Kutokana na mjadala tuliouendesha ni wazi kuwa sera ya serikali kuhusu lugha ya elimu ina mchango mkubwa kichanya au kihasi katika uandishi na uchapishaji. Inaelekea kwamba endapo sera iliyopo sasa ambayo inasisitiza matumizi ya Kiswahili itadumu basi uandishi na uchapishaji kwa Kiswahili utaimarika. Hata hivyo, hali hii itaimarika zaidi iwapo Kiswahili kitapewa nafasi maalumu hasa katika utumishi. Yaani, iwapo mahojiano ya kutafuta kazi nchini yataendeshwa pia kwa Kiswahili na wale wanaojiendeleza vizuri wakipewa mshahara zaidi kuliko wale wasiojiendeleza kwa Kiswahili basi huenda watu wengi wakawa na motisha ya kusoma kwa Kiswahili na hivyo kulipanua soko la vitabu vya Kiswahili mbali na kuikuza haja ya kuandika kwa Kiswahili.

Vifupisho vilivyotumika

CKRC	Constitution of Kenya Review Commission
CPE	Certificate of Primary Education
EAEP	East African Educational Publishers
EAPL	East African Publications Ltd.
GTZ	Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (German Society for Technical Cooperation)
JKF	Jomo Kenyatta Foundation
KCSE	Kenya Certificate of Secondary Education
KIE	Kenya Institute of Education
KIUN	Kiunganishi
KLB	Kenya Literature Bureau
NARC	Ngeli
OUP	Oxford University Press
TEK	Taasisi ya Elimu ya Kenya
TPH	Tanzania Publishing House

Marejeleo

Abdulaziz, Mohamed & Kenneth Osinde 1997. Sheng and Engsh in Nairobi, *International Journal of the Sociology of Language* 125: 1-21.

Altbach, P. G. 1999. The dilemmas of publishing in African Languages: A comparative perspective, in: P. G. Altbach & D. Teferra (eds.) *Publishing in African Languages: Challenges and Prospects.* Chestnut Hill: Bellagio Publishing Network. Pp. 1-10.

Article 19. 1999. *Information Freedom and Censorship: World Report.* London: Library Association Publishing.

Bota, K. N. 2002. *Implementation of the Special Education Curriculum in Kenya; Empirical Study.* Unpublished MA thesis. Hamburg: University of Hamburg.

Callaghan, E. 1997. Is indigenous publishing essential for a developing country such as Kenya to develop culturally?, in: *The Culture of Publishing.* **http://www.brookes.ac.uk/schools/apm/publishing/culture/1997/callagha.html**. 12.08.2000.

Chakava, H. 1992a: Books and reading in Kenya. *Studies on Books and Reading* 13 (UNESCO).

Chakava, H. 1992b. The missing links in the African book publishing chain, *Promoting Technical Publishing in Africa; Seminar Proceedings, 3-6 November 1992.* Arnem, Netherlands: Technical Centre for Agricultural and Rural Cooperation ACPU-EU (CTA).

Chakava, H. 1995. Kenya, in: P. G. Altbach & E. Hoshimo (eds.) *International Book Publishing: An Encyclopedia.* New York: Garland. Pp. 384-396.

Chakava, H. 1996. *Publishing in Africa: One Man's Perspective.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Chakava, H. 1998. A publisher's perspective on children's books. *African Publishing Review* November/ December.

Constitution of Kenya Review Commission. 2002. *The Main Report of the Constitution of Kenya Review Commission* 18th September, 2002.

Githiora, C. Sheng: peer language, Swahili dialect or emerging Creole?, *Journal of African Cultural Studies* 15, 2: 159 – 181.

Heine, B. 1977. Vertical and horizontal communication in Africa, *Afrika Spektrum* 77: 231 – 8.

Hudson, R. A. 1980. *Sociolinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Jwan, J. O. 2004. Pre-primary education in Kenya urban centres. Paper presented at the CODESRIA Institute Dakar.

Kembo-Sure 2000. Suba ethnolinguistic revival. In: R. Voßen, A. Mietzner & A. Meißner (eds.) *„Mehr als nur Worte." Afrikanistische Beiträge zum 65. Geburtstag von Franz Rottland.* Köln: Rüdiger Köppe Verlag. Pp. 639-673.

KIE 2000. *Guidelines for Early Childhood Development in Kenya.* Nairobi: National Centre for Early Childhood Education.

Kiessling, Roland & Maarten Mous. 2001. Urban Youth Languages in Africa. Paper presented at the conference on Language, Migration and the City, 22-24, November 2001. Bayreuth: University of Bayreuth.

Makotsi, R. & L. Nyariki 1997. *Publishing and Booktrade in Kenya*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. 1996. *Language Policy in East Africa.* Nairobi: Education Research and Publication.

Mukuria, D. M. 1995. Kenya's language policy developments with special emphasis on Kiswahili, in: K. Senanu & D. Williams (eds.) *Creative Use of Language in Kenya.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation. Pp. 34-44.

Mulokozi, M. M. 1999. Publishing in Kiswahili: A writer's perspective. In: P. G. Altbach & D. Teferra (eds). *Publishing in African Languages: Challenges and Prospects.* Chestnut Hill: Bellagio Publishing Network. Pp. 11-42.

Mulokozi, M. M. 2002. Kiswahili as a national and international language. Web publication on http://www.helsinki.fi/hum/aakk/documents/kiswahili.pdf (Asian and African Department, University of Helsinki).

Muruguru, S. K. P. 2000. *Students' Performance in Kiswahili: A Study of Selected Schools in Nakuru District, Kenya.* Unpublished MPhil. thesis. Eldoret: Moi University.

Myers-Scotton, C. 1993. *Social Motivations of Codeswitching; Evidence from Africa.* Oxford: Oxford University Press.

Ngesa, Mildred 2002. And Sheng lives on …., *Profile, East African Standard.* February 16-22, 2002.

Nyariki, L. 2000. Bookselling in Kenya, *African Publishing Review* 9, 2.

Odaga, B. A. 1997. Finding the readers in Kenya. *African Publishing Review*, January / February.

Ogechi, N. O. 2001. Publishing in Kiswahili and indigenous languages for enhanced adult literacy in Kenya, *Swahili Forum VIII In Honour of Gudrun Miehe* (*AAP* 68)*:* 185-200.

Ogechi, N. O. 2002a. *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili.* Eldoret: Moi University Press.

Ogechi, N. O. 2002b. Utegemezi au utegemeano baina ya Kenya na Tanzania katika ukuaji na uendelezaji wa Kiswahili nchini Kenya?, *Swahili Forum* IX (*AAP* 72): 155-172.

Ogechi, N. O. 2002c. The African languages dilemma in publishing in Kenya. In: F. R. Owino (ed.), *Speaking African; African Languages for Education and Development.* Cape Town: CASAS. Pp. 329-336.

Ogechi, N. O. 2003. On Language Rights in Kenya, *Nordic Journal of African Studies* 12, 3: 277-295.

Ogechi, N. O. & E. Bosire-Ogechi 2000. Educational publishing in African Languages with a focus on Swahili in Kenya, *Nordic Journal of African Studies* 11, 2: 167 – 184.

Okech, J. G. & A. J. Asiachi 1992. *Curriculum Development for Schools*. Nairobi: Educational Research and Publications (ERAP).

Owino, F. (ed). 1999.Ambivalent adventure: indigenisation of literacy programmes in Africa, in: L. Limage (ed.), *Comparative Perspectives on Language and Literacy; Selected papers from the work of the language and Literacy Commission of the 10th World Congress of Comparative Education Societies, Cape Town 1998.* Dakar: UNESCO.

Owino, F. 2002. *Speaking African; African Languages for Education and Development.* CASAS: Cape Town.

Republic of Kenya 1964. *Report of the Kenya Education Commission.* Nairobi: English Press Limited.

Republic of Kenya 1976. *Report of the National Committee on Educational Objectives and Policies (Gachathi Report)*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya 1981. *The Report of the Presidential Working Committee on the Establishment of the Second University in Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya 1999. *Totally Integrated Quality Education and Training (TIQET). Report of the Commission of Inquiry into the Educational System of Kenya.* Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya 2002. *Ministry of Finance and Planning*. Nairobi: Government Printer.

Rotich, D. C. 1997. Educational publishing and its marketing in developing countries; a case study of Kenya, *The New Review of Information and Library Research* 3: 175-205.

Rotich, D. C. 2000. Textbook publishing in Kenya under a new policy on school textbook procurement, *Publishing Research Quarterly* 16, 2: 60-72.

Thompson, E. J. D. 2001. Transforming the Adult Education Agenda through the Kenya Post-Literacy Project, *Adult Education and Development* 56: 7-19.

Webb, V. & Kembo-Sure 2000. *African Voices: An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa.* Cape Town: Oxford University Press Southern Africa.

Whiteley, W. H. (ed.) 1974. *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Wolff, H. E. 2002. The Heart of the 'African Language Question' in Education. In: Francis Owino (ed). *Speaking African; African Languages for Education and Development.* Cape Town: CASAS. Pp. 129-148.